JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

MISITU NI MALI

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MNADA KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA NA LONGUZA

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza miti aina ya misaji yenye jumla ya meta za ujazo **11,270.847** iliyopo katika mashamba ya miti Mtibwa Mkoani Morogoro na Longuza Mkoani Tanga. Jumla ya meta za ujazo **7,062.230** na **4,208.613** zitauzwa katika shamba la miti Mtibwa na Longuza mtawalia. Miti hiyo iliyopimwa ujazo katika viunga itauzwa kwa mnada kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Miti hiyo ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi za shamba husika. Mnada katika Shamba la Miti Mtibwa utafanyika siku ya **Jumatatu** ya tarehe **29 Machi, 2021** saa **4:30** asubuhi na katika Shamba la Miti Longuza, mnada utafanyika siku ya **Jumatano** ya tarehe **31 Machi, 2021** saa **4:30** asubuhi.

3. Wanunuzi wanakaribishwa kutembelea vitalu shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Meneja wa shamba husika au wasaidizi wake watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada.

4. Mnunuzi mwenye nia ya kushiriki mnada anatakiwa kuwasilisha kwenye bahasha iliyofungwa nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiainisha jina la shamba, namba ya kitalu na pendekezo la bei kwa kila meta ya ujazo anaotarajia kununua kwa kufuata orodha kwenye Jedwali namba 1 na Jedwali namba 2 la Tangazo hili.

5. Uchaguzi wa vitalu (ploti) vya kununua unaweza kufanyika kwa kuzingatia taarifa zilizoorodheshwa katika Jedwali namba 1 na Jedwali namba 2 kama ifuatavyo: -

JEDWALI Na. 1: ORODHA YA VITALU VILIVYOKO SOKONI KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA

Na.	Jina la Kitalu (Ploti)	Meta za Ujazo kwa Kitalu (M^3)	Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/M^3)
1	LR 12-A	307.570	260,000
2	LR 12A-1	205.760	340,000
3	LR 12A-2	229.310	210,000
4	LR 12A-3	207.140	260,000
5	LR 12A-4	217.960	260,000
6	LR 12A-5	144.050	360,000
7	LR 12A-6	218.680	200,000
8	LR 12A-7	242.850	210,000
9	LR 12A-8	210.300	190,000
10	LR 12A-9	235.370	180,000
11	LR 12A-10	201.010	190,000
12	LR 12A-11	303.980	200,000
13	LR 12A-12	103.380	210,000
14	LR 12A-13	204.310	200,000
15	LR 12A-14	115.630	210,000
16	LR 12A-15	193.560	260,000
17	LR14-34	69.440	180,000
18	LR14-36	92.380	210,000
19	LR14-37	132.220	190,000
20	LR14-38	137.760	210,000
21	LR14-39	158.650	210,000
22	LR14-40	231.640	200,000
23	LR14-41	173.420	170,000
24	LR14-42	155.260	140,000
25	LR14 - A	141.890	170,000
26	LR14 - B	193.000	100,000
27	LR14 - C	138.850	140,000
28	LR14 - D	275.950	100,000
29	LR 13-E	102.190	140,000
30	LR 13-F	136.840	170,000
31	LR 13-G	207.230	190,000
32	LR13-I1	412.300	400,000
33	LR13-S	138.770	390,000
34	LR13-T	251.710	450,000
35	LR13-J1	225.670	410,000
36	LR13-K1	264.790	400,000
37	LR13-L1	81.410	400,000
	JUMLA	**7,062.230**	

JEDWALI Na. 2: ORODHA YA VITALU VILIVYOKO SOKONI KATIKA SHAMBA LA MITI LONGUZA

Na.	Jina la Kitalu (Ploti)	Meta za Ujazo kwa Kitalu (M3)	Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/M3)
1	KH5-K1	182.252	770,000.00
2	KH5-K2	153.138	770,000.00
3	KH5-K3	150.808	770,000.00
4	KH5-K4	244.055	770,000.00
5	KH5-K5	264.133	770,000.00
6	KH5-K6	160.033	770,000.00
7	KH5-K13	146.028	770,000.00
8	KH5-K14	150.004	770,000.00
9	KH5-K15	171.467	770,000.00
10	KH5-K16	161.230	770,000.00
11	KH5-K17	167.710	770,000.00
12	KH5-K18	168.400	770,000.00
13	KH5-K20	142.106	770,000.00
14	KH5-K21	130.901	770,000.00
15	KH5-K22	123.280	770,000.00
16	KH5-K23	127.361	770,000.00
17	KH5-K24	157.521	770,000.00
18	KH5-K26	161.808	770,000.00
19	KH5-K27	118.670	770,000.00
20	KH5-K28	168.985	770,000.00
21	KH5-K29	140.394	770,000.00
22	KH5-K30	167.403	770,000.00
23	KH5-K31	111.564	770,000.00
24	KH5-K32	120.392	770,000.00
25	KH5-K33	122.163	770,000.00
26	KH5-K34	125.315	770,000.00
27	KS12 - A24	171.490	720,000.00
	JUMLA	**4,208.613**	

6. Wanunuzi wanatakiwa kufuata Sheria ya Misitu Sura 323 na Kanuni zake za Mwaka 2004 zinazohusiana na uvunaji wa miti na usajili wa kufanya biashara ya mazao ya misitu kabla ya kuanza uvunaji. Hivyo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika kununua miti ya misaji.

7. Wanunuzi wanapaswa kusoma na kuzingatia miongozo ya uvunaji inayopatikana ofisi za shamba husika.

8. Kila Kitalu kitanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi mshiriki wakati wa kufungua bahasha ndiyo itakuwa bei ya kuanzia kunadi kila meta ya ujazo kwa kitalu na bei hiyo haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi.

9. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania utatoa barua ya ushindi kwa mnunuzi aliyeshinda mnada kwa kila kitalu.

10. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50 (1) ya kanuni za misitu za mwaka 2004.

11. Bei za kianzio kwa mita moja ya ujazo zinazooneshwa katika Jedwali namba 1 na Jedwali namba 2 zimejumuisha ‘Royalty’, ‘VAT’, ‘CESS’ na ‘LMDA’.

12. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi kuanzia siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo aliouziwa. Asilimia sabini na tano (75 %) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya mnada. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha baada ya kupewa hati ya madai (bill) ya Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itakayotolewa na Meneja wa Shamba husika au wasaidizi wake.

13. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa meneja wa shamba husika au wasaidizi wake kama uthibitisho wa malipo siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

14. Mnunuzi aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya miezi miwili (**siku sitini**) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100. Aidha, endapo kutajitokeza changamoto ambazo zitasababisha kushindwa kuondoa mazao hayo ya misitu kwa muda uliopangwa, changamoto hizo zitawasilishwa kwa maandishi kwa Meneja wa Shamba husika kwa maamuzi.

15. Usajili wa wanunuzi wenye nia ya kununua na watazamaji utafanyika kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa nne kamili (4:00) asubuhi. Aidha, wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha nia zao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

16. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz.

Limetolewa na
KAMISHNA WA UHIFADHI
S. L. P. 40832
DAR ES SALAAM